Toleo 7

# Ukweli wa Injili


*Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote*

## MAANGAMIZI YA MTU MWENYE HEKIMA

Bwana Mungu akamwambia Sulemani "Omba utakalo nikupe" (1 Wafalme3:5). Badala ya kuomba kupewa utajiri, umaarufu, ama kuishi miaka mingi, Sulemani alimwomba Bwana, "Kwa hiyo nipe mimi mtumwa wako moyo wa adili niwahukumu watu wako, na kupambanua mema na mabaya . . ." (mstari wa 9). Bwana akapendezwa na ombi la Sulemani ndipo akampatia hekima ambayo haikuwahi kuweko wala haitawahi kuweko katika siku sijazo (mstari wa 12). Umaarufu wa Sulemani ukasambaa sana kwa sababu ya hekima yake kuu na uwezo wake mkubwa wa kuelewa mambo.

Sulemani akatajirika na kubarikiwa kwa sababu ya kipawa hiki cha kiungu cha kuwa na hekima. Akajenga hekalu la kuvutia kwa ajili ya kufanyiwa ibada kwa Bwana. Lakini hata ingawa Sulemani alikuwa na hekima kiwango hicho yeye alimuasi Mungu na kuwapenda wanawake wa nchi zingine ambao walikuwa wabudu sanamu. Mungu alikuwa ametoa amri ya wazi: "Bwana aliyowaambia wana wa Israeli, Msiingie kwao, wala wasiingie kwenu; kwa kuwa hakika wataigeuza mioyo yenu kuifuata miungu yao. Sulemani akaambatana nao kwa kuwapenda" (1 Wafalme 11:2).

"Maana ikawa, Sulemani alipokuwa mzee, wake zake wakamgeuza moyo



*Wake wa Sulemani waligeuza moyo wake kufuata miungu mingine.*

wake, afuate miungu mingine, wala moyo wake haukuwa mkamilifu kwa Bwana, Mungu wake, kama moyo wa Daudi baba yake" (1 Wafalme 11:4).

Ni jambo la huzuni kubwa kuoni jinsi Sulemani, ambaye alikuwa na hekima nyingi alivyoangamia. Wakati huo huenda ikawa Sulemani aliamini kwamba alikuwa akifanya jambo la busara la kuoa wanawake wa nchi zingine ili kufanya mapatano ya kisiasa. Yeye akapuuza miongozo ya Bwana huku akishawishika kwamba moyo wake ulikuwa umejitoa kwa Bwana, na kwamba kamwe hangeacha njia ya utakatifu.

Lakini Sulemani hakumgeuka Mungu mara moja. Yeye kwa muda mrefu aliathiriwa na wake zake wa kipagani. Pengine mmoja wa wake zake alimjia na kumwomba pesa za kujenga hekalu kwa ajili ya mungu wake wa kipagani. Hebu mfikirie Sulemani akimjibu ifuatavyo, "Mimi siwaamini hao miungu zako, lakini wewe shika tu hizi pesa unazotaka." Baadaye mke huyo anarudi na kusema, "Ewe Sulemani, kipenzi changu, naomba tafadhali uje katika hafla ya kuwekwa wakfu kwa hekalu la ajabu ambalo umemjengea mungu wangu." Baada ya kushirikiana sana na wake zake ambao hawakumwabudu Mungu wa kweli msimamo dhabiti wa Sulemani dhidi ya

*(Inaendelea kutoka ukurasa 2)*


Tahariri 3

Kujifunza Biblia: Uwezo wa Athari 4

Viwango vya Biblia Kuhusiana na Sinema na Televisheni 5

Viwango vya Biblia Kuhusiana na Sinema na Televisheni 7

Swali na Jibu 9

Je, Wajua?

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu 10

# Mambo Ambayo BIBLIA Inafundisha Kuhusu...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35
**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21
**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10
**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6
**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11
**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8
**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22
**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36
**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18
**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4
**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17
**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16
**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11
**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5
**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46
**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20
**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17
**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Endelea kutoka ukurasa 1)*

uovu ulianza kupungua. Baada ya miaka mingi moyo wake ukaanza kuvutwa mbali na Mungu hadi mwishowe akafanya uovu mbele zake Bwana.

Sulemani alimgeuka Mungu kutokana na athari za wake zake. Hebu basi tujifunze kutokana na hadithi hii yenye msiba mkuu tunapofikiria kuhusu maangamizi yaliyompata mtu huyu ambaye alikuwa na hekima kushinda watu wote. Tunahitaji kuwa makini na kutambua athari ambazo zinaleta misukumo maishani mwetu. Kamwe hatutawahi kufikia kiwango cha juu cha kiroho hivi kwamba tusiathiriwe na athari za uovu hasa ikiwa sisi wenyewe ndio tunajitoa kwa athari hizo kwa hiari yetu wenyewe. Hata ikiwa dhamira zetu ni safi, hata wale wenye uwezo mkubwa wa kiroho kati yetu wataanza kuacha kuwa makini kwa uovu; na kiwango cha kiroho kitaanza kupungua ikiwa utakatifu si jambo tunalolitafuta kwa bidii kabisa maishani mwetu. Hata jiwe hupata shimo ndani yake baada ya maji kuliangukia kwa muda wa miaka mingi.

Shetani hajali itamchukua muda gani kuiba wokovu wetu. Yeye atajaribu kutuchosha kiroho kwa kutumia athari zilizojificha ambazo zimejaa mambo ya ulimwengu. Watu siku hizi wanaacha kuwa macho kwa mambo ya kiroho na wanaruhusu mambo ya kidunia kujaa maishani mwao. Mambo yote unayofanya, mahali pote uendapo, mambo unayosikiliza na utazamayo, hata wale ambao unashiriki nao n.k. yote hayo yana athari maishani mwako. Kumbuka kwamba maangamizi yaliingia maishani mwa Sulemani katika uzee wake. Basi wewe kuwa mwangalifu; daima kuwa mtu wa maombi na uwe macho dhidi ya misukumo na athari ambazo zinakuzunguka.

—mws

## UKWELI WA INJILI

Gazeti la '*Ukweli wa Injili'* huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kusudi la kuimarisha na kuwahimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia ambao umethibitishwa tangu nyakati za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi kutokana na dhambi unaoletwa na utakaso wa Yesu Kristo; ambao hufuatiwa na ujazo wa Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umoja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinafsi na wa upendo ambao msingi wake ni ukweli.

Waandishi: Michael na René Smith

## UAGIZAJI

*Ukweli wa Injili* ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka kwa jinsi Mungu anavyotuongoza. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org ili uagize jalida hili kupitia kwa orodha yetu ya anwani pepe na upokee toleo lako la wakati huu. Hebu jisikie huru kututumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine ambao wangependa kupokea toleo hili kutoka kwa mwandishi wa jalida la Ukweli wa Injili.

## WASILIANA NASI

Gazeti a *Ukweli wa injili* linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimishenari ambazo sisi hufanya huwezekana kupitia kwa matoleo ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.

The Gospel Truth, PO Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@thegospeltruth.org

# Tahariri



*Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa.* —Tito 2:11-12

Hata ingawa dhambi imejaa kila upande Kristo ametoa kila kitu tunachohitaji ili tuweze kuishi maisha matauwa katika ulimwengu huu mwovu wa kisasa. Katika nyakati hizi za tamaa na uovu Mungu ametuita ili tuishi maisha matakatifu. Mzigo ambao Mungu ameweka moyoni mwangu katika robo hii ya mwaka ni kuhusiana na swala la "athari." Athari za ulimwengu huu zinaendelea kupata uwezo zaidi jinsi nyakati zinavyoendelea. Mimi mwenyewe nishawahi kuwasikia Wakristo wa kitambo wakikiri kwamba wanahisi misukumo ya kidunia ikifanya kazi maishani mwao kwa nguvu zaidi kuliko hapo mbeleni. Ndiposa tunahitaji kuwa wenye hekima zaidi na wenye umakini zaidi kuhusiana na athari zinazotuzunguka.

Mimi ninacho kilio kingi moyoni mwangu kwa sababu ya kuona watu wengi wanaokiri kuwa ni Wakristo na ambao walikuwa wamekomaa kwa mambo ya utakatifu sasa wakienenda kama kwamba viwango vya utakatifu ni jambo la kitamaduni tu, na eti sasa "kufanya mambo fulani" silo jambo muhimu. Wazazi wengi wanasukumwa na mienendo ya kidunia, na watoto wao ndio watalipa gharama ile kubwa zaidi. Kuna sababu ya kwa nini watu wengi hawana nguvu za kiroho na hawana upako wa kweli maishani mwao. Tunahitaji kupigia debe viwango vya utakatifu ili tuweze kusimama wima dhidi ya mawimbi ya dhambi ambayo yamekumba ulimwengu.

Athari za kidunia zina  udanganyifu mwingi na inachukua muda mwingi kuona adhari zake maishani mwa watu. Ni jukumu letu kutazama mazingara yanayotunzuguka ili tuone matokeo ya muda mrefu wa athari hizo katika maisha ya watu ambao wameacha kuishi maisha matakatifu. Mimi bado sijaona maisha ya kweli ya kiroho ambayo yanaweza kupatikana katika maisha ya wale ambao wamefungua maisha yao ili kuingia athari za kidunia. Jinsi ulimwengu unavyozidi kuwa mwovu ndivyo kutaendelea kuwa na mgawanyiko mkubwa kati ya watu wa Mungu na watu ambao ni wa jamii zingine. Kamwe hatustahili kujipima kwa viwango za kidunia, bali kwa viwango vya Neno la Mungu.

Katika jalida hili la msimu huu la Ukweli wa Injili, kwa msaada wake Bwana, nimeshughulikia maswala kadhaa yenye mgogoro – mitandao ya intaneti, sinema, televisheni/runinga n.k. Ni jambo muhimu kwetu kutoshikilia sana au kutetea mwelekeo na mawazo yetu. Badala yake tunahitaji kuchunguza nguvu za athari kwa njia ya haki. Ndiposa tunahitaji kufungua mioyo yetu na kuongozwa na Roho Mtakatifu.

Je, wewe mtoto wa Mungu waweza kusema kwa kweli kwamba kila kitu maishani mwako ni kitakatifu na kinakubalika machoni pake Mungu? Je, yawezekana kwamba tayari umekuwa mtu asiye makini kwa maswala ya kiroho? Kazi kuu ya athari za kidunia ni kutufanya sisi Wakristo kuwa na mielekeo ya kuhurumia, kuelewa, na kuvumilia dhambi. Lakini tunahitaji kuwa watu wa kweli na kwa uaminifu tunahitaji kufanya kilio dhidi ya maovu ya ulimwengu.

Michael W. Smith

Januari 2014

*mengi kwa*
MTANDAO

*Tutembelee kwa*

*www.thegospeltruth.org*

*ili uagize na kusoma*

*jarida letu.*



## Athari za Kidunia

*Marafiki Wasioamini*

*Sinema*

*Televisheni*

*Mambo ya Kujiburudisha*

*Muziki*

*Michezo*

*Vyombo vya Habari*

*Kuishi katika Mandhari za Dhambi*

*Kutokuwa na Kiasi*

*Tamaa*

*Uchafu*

*Uganga*

*Pombe*

*Madawa*

"KAMWE HUTAWAHI **KUATHIRI** ULIMWENGU KWA KUJARIBU KUWA KAMA ULIMWENGU."

# MWONGOZO WA KUJIFUNZA BIBLIA

## SOMO: UWEZO WA ATHARI

**Somo la Biblia:** *Chachu kidogo huchachua donge zima.*—Wagalatia 5:9

**Muhstasari:** Adui yetu anatumia athari nyingi zilizojificha ulimwenguni ili kuwavutia watu waachane na utakatifu. Watu wa Mungu wanastahili kutambua ni wapi na ni vipi ibilisi anafanya kazi yake ili waweze kung'oa athari sisizo za kiungu maishani mwao na badala yake kuzibadilisha na athari ambazo ni nzuri na ni za utakatifu.

**Maana:** Athari—nguvu au uwezo wa kubadilisha au kuathiri tabia za mtu au kitu fulani kwa njia isiyo ya moja kwa moja au kwa njia sisizoeleweka; kubadili mwenendo wa mtu.

**I. Kila mmoja wetu anaweza kuathiriwa**
- A. Matendo 14:14-15 Wanadamu wako hali moja.
- B. Zaburi 103:14 Sisi ni mavumbi.
- C. Mathayo 26:41 Mwili ni dhaifu.
- D. Mihali 6:27-28 Moto kifuani.
- E. Mathayo 6:22-24 Huwezi kumtumikia Mungu na mali.

**II. Mifano ya Biblia**
- A. Mwanzo 3:1-8 Adamu na Hawa.
- B. Waamumuzi 16:18-20 Samsoni.
- C. 1 Wafalme 11:4 Solomoni.
- D. Luka 22:55-62 Petro.

**III. Kuwa Macho**
- A. Wagalatia 6:7-8 Unavuna unachopanda.
- B. Isaya 5:20-22 Kuita uovu wema.

**IV. Uwezo wa Mambo Madogo**
- A. 1 Wakorintho 5:6 Chachu kidogo.
- B. Wimbo wa Sulemani 2:15 Mbweha wadogo.
- C. Mhubiri 10:1 Mainzi mafu.

**V. Athari Zenye Kuleta Uovu**
- A. Wagalatia 5:19-21 Matendo ya mwili.
- B. 1 Wakorintho 15:33 Urafiki mbaya.
- C. 2 Wakorintho 6:14-17 Wasioamini.
- D. Mithali 7:7-26 Tamaa.
- E. Waefeso 5:18 Mvinyo.

**VI. Zikatae Athari Sisizo za Kiungu**
- A. Mithali 4:14-15 Usiingie.
- B. 2 Timotheo 2:22 Toroka tamaa za ujana.
- C. Waefeso 5:6-13 Wape onyo.
- D. Zaburi 141:4 Usiuelekeze moyo wako.
- E. Waefeso 4:27 Usimpe Shetani nafasi.
- F. Yakobo 4:7-8 Mpingeni Shetani.

**VII. Tunza Akili na Moyo Wako**
- A. Mithali 4:23 Tunza moyo wako.
- B. Mathayo 5:29-30 Jicho lako likikukosesha.
- C. Zaburi 101:3 Sitaweka mbele ya macho yangu neno la uovu.
- D. Waebrania 12:13-15 Tafuteni utakatifu.
- E. 1 Wakorintho 6:12 Si vitu vyote vifaavyo.

**VIII. Athari zenye Kuleta Faida.**
- A. Waebrania 10:24-25 Kukutana pamoja.
- B. 1 Yohana 1:5-7 Ushirika.
- C. Mithali 27:17 Chuma hunoa chuma.
- D. Zaburi 119:11 Neno la Mungu.
- E. Zaburi 1:1-2 Amebarikiwa.

**Tamati:**
*Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.*
—Warumi 12:2

# UWEZO WA ATHARI

*Nakala ya kuandamana na Mafunzo ya Biblia*

### ADUI WA NAFSI ZETU YUMO KAZINI

Shetani anafanya vita dhidi ya watu wa Mungu. Kusudi lake kuu ni kuangamiza kiini cha maisha yao ya kiroho. Adui huyu ni mjanja na anajua udhaifu wetu wote. Hata ingawa mtu kujaribiwa kutenda dhambi ni jambo la kawaida, wakati mwingi hatari ile kubwa zaidi katika maisha ya Mkristo huwa ni athari ambazo zinafanya kazi dhidi ya watoto wa Mungu.

### KILA MMOJA WETU ANAWEZA KUATHIRIKA

Athari ni uwezo wa kubadilisha tabia ama sifa za mtu. Mradi mwanadamu angali yumo mwilini daima atakuwa akiathiriwa na uwezo wa athari tofauti. Mtume Paulo na Barnaba walitangaza kwamba “Sisi nasi tu wanadamu hali moja na ninyi” (Matendo 14:15). Ndiposa Yesu aliwaonya wanafunzi wake “Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu” (Mathayo 26:41). Basi wewe usiwe mpumbavu kuhusu uwezo wa athari za uovu. Wakristo wengi ni washirika wa shughuli za kidunia na anasa ambazo ndani yake kumeingizwa upotovu wa dhambi. Na bado wao hushangaa ni kwa nini hawana ushindi na uwezo ndani yake Mungu: “Je! Mtu aweza kuua moto kifuani pake, na nguo zake zisiteketezwe?” (Mithali 6:27).



*Mradi mwanadamu angali yumo mwilini daima atakuwa akiathiriwa na uwezo wa athari tofauti.*

### MIFANO YA BIBLIA

Maandiko ina mifano mingi ya watu mashujaa ambao waliangushwa na uwezo wa athari za uovu. Hapo mwanzo Adamu na Hawa walipoteza usafi na heshima zao kwa Mungu kwa sababu walisikiliza uongo na hadaa za nyoka (Mwanzo 3:1-8). Samsoni naye alifanya michezo ya kimapenzi na Delila na hakutarajia kumwambia Delila siri ya nguvu zake nyingi (Waamuzi 16:18-20). Kuna athari ambazo zinafanya kazi maishani mwetu ambazo polepole zitapunguza misimamo yetu dhidi ya uovu mpaka ifike wakati ambapo kwa ajili ya udhaifu tunatenda dhambi. Sulemani alimgeuka Mungu katika uzee wake kutokana na athari za wake zake (1 Wafalme 11:4). Naye mtume Petro alimkana Bwana kwa sababu ya misukumo ya umati wa watu (Luka 22:55-62). Wengi wameacha njia ya utakatifu kwa kujifunga na athari za kidunia na kwa kukosa kuwa na misimamo thabiti dhidi ya athari hizo.

### UWEZO WA MAMBO MADOGO MADOGO

Athari ndogo huwa na uwezo mwingi: “Hamjui kwamba chachu kidogo hulichachusha donge zima?” (1 Wakorintho 5:6). Wakati mwingi ni “Wale mbweha wadogo ndio waiharibuo mizabibu” (Wimbo wa Sulemani 2:15). Kusema kweli sio dhambi kubwa hufanya Wakristo kupoteza wokovu wao bali ni athari zile ndogo sisizoonekana ndizo huanza kuathiri mawazo na mielekeo ya utakatifu wa ukweli. Lakini wewe unasema, “Hii si dhambi. Naweza kwenda huko. Naweza kusikiliza muziki huo. Naweza kutazama sinema hiyo. Mimi nimeokoka na sitofanya chochote kibaya.” Maneno kama hayo wakati mwingi huwa ndio ya kwanza kuongoza watu kwa njia ya kuanguka. Tafakari kuhusu athari ya mambo haya maishani mwako. Je, yanaathiri vipi maisha yako ya kiroho. Je, wewe wajihisi kwamba kuna msukumo kwako kufanya mambo ambayo hayafai? Je, unajaza akili zako mambo ambayo si safi na matakatifu? Basi kuwa mtu mwenye hekima ili upate kujua uwezo wa mambo madogo.

### ATHARI ZA UOVU ZIMEJAA KOTE

Kazi za kimwili—uzinzi, uasherati, uchafu, uabudu sanamu, uganga, wivu, ulevi n.k. (Wagalatia 5:19-21)—zimejaa kote ulimwenguni. Athari hizi zimeingia katika fani za muziki, mambo ya kujiburudisha, michezo, n.k. Mtoto wa Mungu hawezi kuruhusu athari za uovu maishani mwake bila kupatwa na matokeo mabaya katika maisha yake ya kiroho. Maandiko yanatufunza kwamba “Msidanganyike! Urafiki mbaya huharibu tabia njema” (1 Wakorintho 15:33 BHN).

*(Inaendelea kutoka ukurasa 6)*

*(Endelea kutoka ukurasa 5)*

Ikiwa mtu atakuwa na ushirika wa karibu na watu wasio watakatifu, baada ya muda atapata udhaifu wa kiroho na imani yake na utakatifu wake utaingiwa na dosari. Hii ndio sababu onyo limetolewa kuwa "Msiambatane na watu wasioamini" (1 Wakorintho 6:14). Basi ni muhimu kabisa mtu kuwa makini sana anapochagua marafiki zake wa karibu na hasa mwenzake wa ndoa.

### Kataa uovu

Maandiko yanasema kwamba tunahitaji kukataa uovu kabisa na kujitenga na athari za dhambi: " Usiingie katika njia ya waovu . . . Jiepushe nayo, usipite karibu nayo, Igeukie mbali, ukaende zako" (Mithali 4:14-15). Kemea kazi za uovu (Waefeso 5:11). Kuna watu wengi ambao husema hakuna makosa kushiriki mambo fulani maishani ambayo hayajakatazwa moja kwa moja na kuitwa dhambi. Lakini mtoto wa Mungu ambaye atakuwa mwaminifu hadi mwisho ni Mkristo yule ambaye atachukua msimamo dhabiti dhidi ya athari zote za uovu na ambaye hampatii ibilisi nafasi hata kidogo (Waefeso 4:27). Jinsi ambavyo mtu anadumisha kiwango kikubwa na kuweka umbali kati yake na athari mbaya ndivyo ambavyo athari hizo hukosa nguvu za kufanya kazi mwilini mwake: "Lakini zikimbie tamaa za ujanani; ukafuate haki, na imani, na upendo, na amani, pamoja na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi" (2 Timotheo 2:22).



*Lakini mtoto wa Mungu…atachukua msimamo dhabiti dhidi ya athari zote za uovu na ambaye hampatii ibilisi nafasi hata kidogo.*

### Tunza mawazo na moyo wako

Tunza mawazo na moyo wako kutokana na uwezo wa dhambi na usipatie nafasi mambo ambayo yanaweza kuleta hali ya kutokuwa na utakatifu: "Lakini zikimbie tamaa za ujanani; ukafuate haki, na imani, na upendo, na amani, pamoja na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi" (Mithali 4:23). Kama Daudi alivyosema, "Sitaweka mbele ya macho yangu neno la uovu…" (Zaburi 101:3). Dumisha maisha yako na nyumba yako kama hekalu linalofaa kwa Roho Mtakatifu. Kama kuna jambo ambalo lina athari mbaya kwa maisha yako ya kiroho unahitaji kuling'oa hata ikiwa Wakristo wengine wanashiriki jambo hilo: "Jicho lako la kuume likikukosesha, ling'oe ulitupe mbali nawe…" (Mathayo 5:29-30). Sio lazima kitu kiwe ni dhambi. Zingatia kuhusu uwezo wa athari zake. Kama mtume Paulo alivyosema, "Vitu vyote ni halali kwangu, lakini si vyote vifaavyo; vitu vyote ni halali kwangu, lakini mimi sitatiwa chini ya uwezo wa kitu cho chote" (1 Wakorintho 6:12).

### Athari nzuri

Badala ya kuwa katika hali ya hatari kutokana na athari za kidunia tunahitaji kutafuta utakatifu (Waebrania 12:13-15) na pia kutafuta mambo ambayo yatatujenga na kuleta athari nzuri maishani mwetu. Unahitaji kuwa na ukakamavu na kuwa mwaminifu katika ushirika wa watu wa Mungu bila kikomo (Waebrania 10:24-25). Yajaze maisha yako na shughuli na utumishi ambao unakuza ukuaji wako wa kiroho. Waruhusu watu watakatifu waathiri maisha yako na hasa uruhusu Neno la Mungu kukuathiri: "Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, nisije nikakutenda dhambi" (Zaburi 119:11).

### Chaguo ni lako

Kuna athari nyingi zenye uwezo mkubwa ambazo zimemzunguka Mkristo, lakini kila mtoto wa Mungu ana uchaguzi wa kile ambacho ataruhusu kiingie maishani mwake. Ombi letu ni kwamba wewe utachagua athari ambazo zina manufaa na za utakatifu kuingia maishani mwako: "Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu" (Warumi 12:2).

—mws

*Mwongozo wa Biblia Kuhusu*

# Sinema na Televisheni

Kiwango cha Biblia kuhusiana na utazamaji wa sinema na televisheni kinaweza kutajwa kwa neno moja tu: utakatifu. Utakatifu ni mtu kuwa safi, asiye na dosari, aliyetakaswa, aliyetengwa kwa ajili ya Mungu, mnyoofu katik mambo yote maishani mwake. Maandiko yanatufundisha kwamba "mtukuzeni Mungu katika miili yenu" (1 Wakorintho 6:20). "Maana Mungu hakutuitia uchafu, bali tuwe katika utakaso" (1 Wathesalonike 4:7). Bila utakatifu "hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao" (Waebrania 12:14). Basi mtu anahitaji kutambua uwezo wa athari za sinema na televisheni na kupima athari hizo dhidi ya maandiko ambayo tumeyataja hapo juu. Kama watoto wa Mungu tumeagizwa "fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu" (1 Wakorintho 10:31).

Ufundi ambao huunda vifaa vya sinema na televisheni/runinga, na waya ambazo zinaunganisha mitambo hiyo hazitokani na nia ya (kutenda) dhambi. Shida huwa ni yaliyomo kwenye vipindi vya televisheni au sinema na athari za muda mrefu ambazo vipindi hivyo vinaweza kumletea mtu. Siku hizi televisheni na sinema zimejaa uchafu na ukosefu wa utakatifu. Wagalatia 5:19-21 inataja msururu wa matendo ya kimwili: "uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, . . . watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu." Sinema zimejaa picha za mambo ya kimwili ambayo yametajwa hapo juu. Je, ni kwa nini mtoto wa Mungu mwenye shauku ya kuishi maisha matakatifu ajaze moyo na akili zake mambo ambayo kwa si ya kiungu?



**Je, ni kwa nini mtoto wa Mungu ambaye ana shauku la kuishi maisha matakatifu ajaze moyo na akili zake mambo ambayo kwa kweli si ya kiungu?**

Nyumba ya Mkristo inahitaji kuwa ngome na mahali pa utulivu dhidi ya uchafu wa dunia. Kuna athari za kutosha na nguvu za kimwili ambazo zimo ulimwenguni hata bila kuzileta nyumbani mwetu kulisha nafsi zetu nazo. Sinema na yaliyomo kwenye vipindi vya televisheni zinaweza kuvutia mwili lakini tumeitwa ili tusulubishe mwili na tamaa zake na mambo mengine ambayo mwili unapenda na badala yake kutembea kwa Roho. Maandiko pia yanaongoza mwili wa Kristo kuhusu kile ambacho wanastahili kuwaza: "Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo" (Wafilipi 4:8).

Mambo haya huwa dhahiri kabisa kwa mioyo ya kweli yanapopimwa kulingana na Neno la Mungu. Je, mtu huwa ametenda dhambi kwa sababu tu ya kutazama sinema fulani? Hapana; lakini mtu akizingatia uwezo wa athari sisizo takatifu na ambazo ndizo huongoza nyingi za sinema na vipindi vya televisheni ingekuwa bora zaidi kwa mtu kujinyima athari kama hizo. Adui yetu ametumia athari kubwa za sinema na televisheni na kuzifanya kuwa za kuleta hasara kubwa kwa mambo ya kiroho na za kitabia kwa vizazi vingi. Vyombo vya habari huwa na malengo yake na si jambo ngumu mtu kutambua filosofia za uovu na aina ya maisha ambayo yanapigiwa debe na vyombo hivyo vya habari.

Mara nyingi takwimu na utafiti zimedhibitisha kuhusu athari mbaya ambazo utazamaji wa televeshi huleta kwa watoto. Asilimia kubwa ya sinema na vipindi vya televisheni vimejaa tabia ambazo si za kiungu. Tabia hizi huleta madhara makubwa kwa watoto na zinaweza kuwaletea tabia mbaya kama vile za utumizi wa mabavu, kufanya kuwa wachokozi, matumizi ya madawa ya kulevya, tabia mbaya za kingono, miili yao kuwa na kipimo cha uzito uliopita kiasi, kujiona kwamba hawafai, na kutofanya vyema shuleni. Kiwango kile ambacho mtoto anaruhusiwa kutazama vipindi vya "kawaida" kwenye televisheni ndicho kiwango ambacho mtoto huyo atajaribu kuiga mambo ambayo anaona.  Nyingi za sinema huonyesha hali ya maisha ambayo si ya kawaida na pia huonyesha kwamba mtu hapati matokeo ya matendo yake maovu. Jambo hili hufanya watoto kufuata tabia ambazo anaona katika televisheni. Vipindi hivyo pia hufanya watoto kutukuza tabia sisizofaa na kufanya dhambi kuonekana kitu cha kupendeza na ambacho kinakubalika.

Watu wote, hasa watoto na vijana, huvutiwa sana na mambo ambayo wanaona na kutazama. Mimi ninakumbuka

*(Inaendelea kutoka ukurasa 8)*

*(Endelea kutoka ukurasa 7)*

nikizungumza na kijana mdogo katika mkutano wa kanisa ambaye alishangaa sana kwamba nilisafiri kwenda kwa mkutano huo kwa ndege. Akaniambia, “Mimi kamwe siwezi kufanya hivyo.” Yeye aliogopa ndege kwa sababu alikuwa ametazama sinema ya kuogofya kuhusu nyoka na ndege. Pia akasema hangependa kusafiri kwa gari la moshi kwa sababu ya kitu kingine ambacho alikuwa ametazama. Basi tunahitaji kuwa waangalifu na kutambua uwezo mkubwa wa sinema.

Lakini watu wengine husema, “Mimi hutazama tu sinema na vipindi vizuri.” Pengine hilo ni jambo la kweli, lakini tukichunguza swala hilo kwa makini, je, sinema hizo ni takatifu. Je, kuna baadhi ya maneno ama sehemu yake ambayo unakosa kutilia maanani ama unalazimishwa kutazama upande mwingine yanapofanyika? Je, sinema au vipindi hivyo vinapoteza wakati mwingi na kuduwaza hisia zako za kiroho. Wakati mtu anatazama sinema kwa muda mrefu bila kukoma yeye hupata shauku na kiu cha kutazama sinema zingine. Kitu ambacho kilianza kimchezo kinaweza kubadilika na kuwa jambo la “kukushika kabisa” na kukufanya uzidishe viwango vya sinema ambazo unaweza kutazama.



**Wakati mtu anatazama sinema kwa mfululizo**

**bila kukoma yeye hupata shauku**

**na kiu cha kutazama sinema zingine.**

Watu wengi wazuri wameanza kutazama sinema ambazo wanaona zinafaa; lakini baada ya muda, kama hawako makini kwa sauti ya Roho, wanaruhusu mambo mengine yasiyo ya kiroho kuingia maishani mwao. Inakuwa vigumu kwao kuwa na viwango vya kudumisha na wanaona vigumu kuacha kutazama sinema hizo. Inakuwa ni kwa rehema za Mungu tu ndivyo wanazinduka na kutambua kile ambacho wamejiruhusu kutazama. Televisheni nayo hasa hutumiwa kama kitu cha kuburudisha watu, na ndani mwake kumejaa tamaa za mwili, tamaa za jicho, na kiburi cha maisha. Mambo haya hayatokani na Mungu na yanahitaji kukataliwa maishani mwetu. Matangazo mengi ya biashara ambayo hufanywa kwenye televisheni katikati mwa vipindi vinavyosemekana kuwa bora vinatosha kumwaibisha mtoto wa Mungu. Wakati athari za mambo haya zinapozidi mtu anayetazama mambo haya hufa ganzi kiroho na anakosa kutambua uovu huo. Jambo hili nalo huanza kudunisha kanuni za ukweli na utakatifu wa moyo. Athari hizi zimekuwa mtego mkubwa wa kunasa Wakristo wengi. Basi wewe Mkristo unahitaji kuwa macho!

Sinema zimechukua muda mwingi ambao Mungu angehitaji utumike katika huduma yake na ibada kwake. Kutazama sinema na televisheni ni mambo yanayoathiri uwezo wa mtu wa kuwa makini na pia kumuongezea uchovu. Pia inafanya hisia za mtu kufa ganzi. Inakuwa vigumu mtu kusoma na kuomba. Pia inakuwa vigumu mtu kuwa makini darasani ama kwenye ibada za kanisa.

Televisheni na sinema ni vitu ambavyo vimetumika kusambaza uovu ulimwenguni. Mimi mwenyewe nimeona athari ya mambo hayo katika tamaduni za nchi ambazo hazijaendelea sana. Nimetazama “dhambi za nchi za ulaya” zikisambazwa kwenye nchi hizi kupitia kwa nyanja za kujiburudisha. Wakristo katika baadhi ya nchi hizo wanatambua uovu na uwezo wa athari za televisheni katika maisha ya watu wanaowazunguka. Watu wanaanza kukosa kiasi katika mavazi na matendo yao, na mambo yanayoonekana kwenye televisheni ndio huanza kupewa sifa, halafu watu wanaanza kujaribu kufuata mfano wa mambo wanayoona kwenye televisheni yakifanywa mambo “ya kisasa” ya kujifurahisha. Lakini Mungu ametuita kuishi maisha matakatifu na tunahitaji kuweka vizuizi kati yetu na uovu ambao umevuma sana siku hizi.

Hebu tuseme tena, kiwango cha Biblia kuhusiana na kutazama sinema na televisheni ni kipi? Wewe mwenyewe fanya uamuzi mbele zake Mungu na Neno lake. Neno kuu katika jambo hili ni utakatifu. Shida sio kifaa kile kinachotumika (mkanda wa sinema, video, DVD, televisheni, au mtandao wa mawasiliano wa intaneti) bali ni uwezo wa athari wa kile ambacho unatazama. Kuwa mwangalifu na mwenye hekima.

Watoto wa Mungu wameitwa ili wawe mfano bora na kuwa nuru ya ulimwengu. Kanuni hii peke yake inastahili kututahadhari ili tuwe waangalifu kwa mambo yale ambayo tunaruhusu maishani. Viongozi na wahudumu wa injii wanahitaji kuishi kwa viwango dhahiri vya utakatifu na uungu.

Mfalme Daudi alisema kwa njia sawa na ya ukweli katika Zaburi 101:3: “Sitaweka mbele ya macho yangu neno la uovu. Kazi yao waliopotoka naichukia, haitaambatana nami.”

—mws

# SWALI na JIBU

**Swali:** Je, mtandao wa intaneti unastahili kuwa na sehemu gani katika maisha ya Mkristo?

**Jibu:** Maswali mengi yameulizwa ikiwa Mkristo anastahili kuwa na mtandao wa intaneti, na pia swali kwamba mtandao wa intaneti unastahili kuwa na sehemu gani katika maisha ya Mkristo. Je, tofauti kati ya mtandao wa intaneti na televisheni ni ipi? Je, kuna viwango mbili tofauti kuhusiana na maswala haya mawili?

Ni muhimu kutambua tofauti iliyoko kati ya televisheni na mtandao wa intaneti. Kusudi kuu la televisheni ni kuburudisha, aidha kupitia kwa sinema au michezo.

Kwa upande mwingine intaneti ni mtandao unaounganisha habari tofauti tofauti kote ulimwenguni. Intaneti inatumika kikazi, kuwasiliana, kufanya utafiti n.k. Hiki ni kifaa cha ajabu chenye msaada mkubwa, lakini pia kinatumika kwa uovu mwingi. Intaneti inamruhusu mtu kupata filamu na vipindi vingi ambavyo havionyeshwi kwenye televisheni. Hii ni kusema kwamba intaneti ina uwezo mkubwa zaidi wa kuleta uovu kuliko kitu chochote ambacho televisheni ishawahi kuwa nacho. Lakini kungali kuna tofauti kati ya mambo hayo mawili. Mtu anaweza kuongoza intaneti kuhusu kile ambacho anaweza kupata kutokana nayo hata kuliko jinsi ambavyo anapata kutoka kwa televisheni, ambayo huongozwa na wale humiliki, na ambao ndio huleta vipindi. Kwa upande mwingine uovu wa hali ya juu kabisa uko mikononi mwa wanaotumia intaneti. Kwa sasa si lazima watu kwenda mahali palipojificha ili kutimiza tamaa zao za mwili. Wanaweza kutimiza hayo yote humo nyumbani mwao kwa njia ya intaneti. Ndiyo sababu tunasema kwamba intaneti ina uwezo mkubwa na inaweza kuwa hatari sana.

Basi mafundisho kuhusiana na utakatifu yanahitaji kutumika katika matumizi ya kifaa hiki cha intaneti. Kama kitatumika kama kifaa cha kujiburudisha basi kinaweza kukiuka mipaka ya utakatifu. Intaneti imekuwa sasa kifaa cha kuwezesha watu kuhepa hisia zenye uchungu na hali ambazo zinawasumbua. Watu wametumia masaa mengi ya kulala huku wakiwa kwenye mitandao ya intaneti. Wengi huacha ushirika na familia



zao na hata marafiki na badala yake wanapata kitulizo katika ulimwengu wa intaneti ambao wao wenyewe wamejiundia na kuongoza.

Intaneti ni kama bunduki yenye risasi. Sio kitu cha kuchezewa bali ni kitu cha kutumiwa kwa uangalifu na kwa umakini kama kifaa hatari lakini ambacho kina manufaa pia. Kunao watu ambao hawastahili kutumia au kuwa na bunduki. Mambo yako hivyo pia katika matumizi ya mtandao wa intaneti. Kuna watu ambao wanastahili kujitenga nayo kabisa kwa ajili ya usalama wao na ulinzi wao dhidi ya udhaifu wao.

Kama intaneti inatumiwa vizuri inaweza kuleta manufaa mengi. Basi wewe idumishe intaneti iliyotakaswa. Wakati mwingi watu wametilia maanani intaneti hata kuliko wakati wa ibada zao za kibinafsi na intaneti inakuwa kitu cha kupoteza wakati. Watu hupata hashuo kubwa kwa kutumia intaneti sana na wanakuwa "walevi" wa habari nyingi. Basi tunahitaji kuwa na kiasi kwa matumizi yake na tunahitaji kuchunguza tena matumizi yake nyumbani.

Mitandao ya kijamii inaweza kuwa muhimu kwa maswala ya kiroho na pia kwa ajili ya kupatana na marafiki. Lakini pia kitu hiki kinaweza kuwa cha hatari sana kinapotumiwa vibaya. Kuna nyumba nyingi ambazo zimevunjika kutokana na kile ambacho kilianza kama mawasiliano ambayo hayana nia mbaya. Jambo hili pia limefanya vizuizi vilivyomo kati ya vijana na hata kati ya wazee kutupiliwa mbali, vizuizi ambavyo Bwana angependa zidumishwe.

Kama vile ambavyo bunduki yenye risasi inahitaji kuwekwa mahali salama, hivyo ndivyo matumizi ya mtandao wa intaneti manyumbani. Watoto wanahitaji kuangaliwa kwa makini sana ikiwa watatumia intaneti kwa ajili ya matumizi ya shule au kwa ajili ya kufanya utafiti. Ni vizuri mzazi kutumia kifaa cha kuongoza yaliyomo kwenye intaneti ili kuzuia yale ambayo mtoto anaweza kusoma au kutazama katika mtandao huo kwa ajili ya kuwakinga dhidi ya majaribu.

Tunaishi katika nyakati za teknolojia ambapo mtandao wa intaneti umefanyika kifaa muhimu sana. Lakini tunahitaji kutambua hatari iliyoko kwenye kifaa hiki. Nafsi yako ndio kitu muhimu zaidi kuliko mambo mengine chote. Basi hebu maamuzi yako yadhihirishe ukweli huo na utakatifu, kiasi, na umakini ukuongoze kila wakati ambapo unatumia intaneti.

—mws

## JE, WAJUA?

**Muziki una athari kubwa kwa wanadamu.**

Muziki hudhihirisha hisia tofauti za mwanadamu, jinsi wanavyojisikia, na pia unaweza kufanya watu kuwa na hisia za furaha, huzuni, hasira, n.k. Aina tofauti za muziki na maneno yanayotumika na hata mdundo wake unaathiri jinsi watu wanavyojihisi na mielekeo yao kuhusiana na ulimwengu. Watu wengi hukimbilia kwenye muziki ili kupata kitulizo cha moyo na ili kuondoa upweke uliomo ndani yao. Muziki pia unaweza kutumika kumsaidia mtu katika ibada zake na pia unaweza kumfanya mtu kutoroka ulimwengu wake.



**Je, muziki huwa na sehemu gani maishani mwako?** Je, muziki unaosikiliza ni mzuri, usio na uchafu, na wenye utakatifu ndani yake? Je, muziki huo hujaza pengo ndani yako ambalo Mungu angependelea kuliziba mwenyewe.

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# Vita si Vyako

*Bwana awaambia hivi, Msiogope, wala msifadhaike kwa ajili ya jeshi kubwa hili; kwani vita si yenu bali ni ya Mungu.* —2 Mambo ya Nyakati 20:15b

Yehoshafati alisikia habari kuhusu jeshi kubwa lenye nguvu likija kufanya vita dhidi yake. Basi akakiri mbele zake Bwana "sisi hatuna uwezo juu ya jamii kubwa hii, wanaotujia juu yetu; wala hatujui tufanyeje; lakini macho yetu yatazama kwako" (mstari wa 12).



Shetani anafanya kazi kila upande akijaribu kushusha mioyo ya watu wa Mungu. Ibilisi hasa anafanya juhudi dhidi ya wahudumu wa kweli wa injili ambao wamejazwa Roho Mtakatifu ambao wanajinyima yote kwa ajili ya injili. Kuna matukio mengi ambayo hutujia ambayo vita tunavyopigana huonekana kuwa kubwa sana kutushinda na kwamba hali zake zitatuangusha. Lakini sisi tu salama tunapokiri upungufu wetu kama jinsi Yehoshafati alifanya na kwa kukazia macho yetu kwa Mwokozi wetu.

Habari njema ni kwamba Roho wa Mungu alimpatia Yehoshafati ujumbe ule ule ambao Bwana anawapatia watu wake leo: "Usiogope. Vita hivi si vyako, ni vya Mungu." Sisi hupata amani nyingi moyoni tunapotambua kwamba Mungu ameshika usukani na kwamba hatuna majibu yote na hata hatuna uwezo wa kushinda kundi hili kubwa linalotuzunguka kwa nguvu zetu wenyewe.

Yehoshafati akaambiwa: "Simameni, mkauone wokovu wa Bwana" (mstari wa 17).

Hebu basi tusimame wima na tupate tulizo na hakikisho kwamba Mungu atawatunza watu wake.

—mws

**Anwani**

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA